

KINA CHA FIKIRA



KAULI YA WALIBORA

"Nimefurahi kupata nakala zangu za awali za tafsiri ya riwaya yangu Siku Njema kwa Kiswahili. Kiswahili kinaendelea kutoa, si kupokea tu."

BAADHI ya vitabu bora nilivyowahi kusoma havikuandikwa kwanza katika lugha ninayoelewa. Mathalani nilikumbana na riwaya za mwandishi Mrusi Leo Tolstoy kama vile *War and Peace* na *Anna Karenina* nikakorwa na ubora wa kisanii. Lakini Tolstoy aliziandika riwaya zake katika Kirusi nisichokijua.

Hizi riwaya za ragha kubwa zinazosheheni maudhui mbalimbali yakiwemo mahaba na vita, zimenifikia mimi na wengine wengi kwa sababu ya mzungu wa tafsiri. Nasisitiza kwamba tafsiri ni mzungu, tena mkubwa sana kwa maana unafanikisha mawasiliano kati ya lugha mbili mfaraka, kila lugha ikifumbatwa na kanuni miundo na tamaduni zinazokinzana na nyingine.

Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Kambarage Nyerere naye alifanikiwa kutuletea ukwasi wa ubunifu wa William Shakespeare kwa kuzitafsiri kazi zake mbili kwa Kiswahili, yaani *Juliasi Kaizari* na *Mabepari wa Venisi*. Nakumbuka furaha yangu kuzisoma kazi hizi za Shakespeare kwa Kiingereza; yaani *Julius Caesar* na *Merchants of Venice* na kuzilinganisha na tafsiri ya Mwalimu Nyerere.

Kama anavyodai Prof Alamin Mazrui, ni kupitia kwa tafsiri ambapo kazi za fasihi kutoka kwingineko zilijumuishwa katika fasihi ya Kiswahili. Hata katika mfumo wa elimu, wakati vitabu vya kutahiniwa vilivyoteuliwa kwa ajili ya somo la fasihi ya Kiswahili, zilikuwamo tafsiri za Kiswahili kama vile *Mfalme Edipode*, tafsiri ya Samuel Mushi ya tamthilia ya Myuyani Sofokile itwayo *Oedipus Rex* au *Oedipus the King*. Hata tafsiri za Nyerere za kazi za Shakespeare ziliingia katika tapo la fasihi ya Kiswahili.

Kutafsiriwa kwa kazi za kwingineko kwa Kiswahili ni jambo zuri. Mwanzoni hilo tu ndilo lililokuwa likifanyika. Hata maandiko matakatifu kama vile Biblia na Kurani yalitafsiriwa kutoka kwa lugha hizi hadi kwa Kiswahili kwa ajili ya hadhira za Kiswahili.

Hata hivyo, haki inasema haifai tafsiri kuenda upande mmoja pekee; kutoa ni kikoa, ukipokea nawe toa.

RIARA UNIVERSITY LIBRARY
P. O. Box 49940 - 00100,
NAIROBI



Fahari iliyoje Fasihi ya Kiswahili nayo pia kutafsiriwa!

Kwa hivyo, juhudi za kutafsiri kazi za Kiswahili kwa lugha nyingine za dunia zimekuwa zikifanywa, nazo zinastahili kupongezwa. Ebrahim Hussein, mathalani, alitafsiri tamthilia yake ya *Kinjeketile* kwa Kiingereza naye Kimani Njogu akamtafsira *Mashetani* kwa Kiingereza pia.

Baadhi ya kazi za Shaaban bin Robert zimetafsiriwa kwa Kijerumani, Kifaransa na Kiitaliano. Vile vile, zipo kazi za Said A. Mohamed ambazo nazo zimetafsiriwa kwa lugha kadha za Ulaya. Mathalani tamthilia ya *Amezidi* ambayo ilitafsiriwa kwa Kiingereza

kuwa *He is too Much*.

Nilikuwa siku zote nikitarajia kazi yangu moja muhimu itafsiriwe ili wasomaji wa lugha nyingine wafaidi uhondo. Baraza la Kiswahili la Taifa (Bakita) lilitafsiri hadithi yangu ya Kiingereza *Bobby the Dog* hadi kwa Kiswahili nikafurahi sana. Nami mwenyewe katika unyonge wangu nilijikusuru kutafsiri hadithi ya watoto ya *Ndoto ya Amerika* hadi kwa Kiingereza.

Na sasa nimefurahi kupata nakala zangu za awali za tafsiri ya riwaya yangu *Siku Njema* kwa Kiswahili. Kiswahili kinaendelea kutoa, si kupokea tu.